

JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA SUMBAWANGA
SHULE YA SEKONDARI MPUI

Shule ya Sekondari Mpui,
S.L.P 338,

SUMBAWANGA

Tar.....

Namba za simu

Mkuu wa Shule: **0763445546/0621124185**

Makamu Mkuu wa Shule; **0766493028**

Matroni: **0757216207**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

.....
S.L.P

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MPUI KIDATO
CHA KWANZA 2021

1. Nafurahi kukujulisha kuwa mwanaoamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021**.
Shule ya sekondari Mpui ipo umbali wa **kilometa 55** mashariki mwa mji wa Sumbawanga. Usafiri wa mabasi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Sumbawanga kwa wanafunzi watokao nje ya eneo la kata ya Mpui Muhula wa masomo unaanza **11. 01.2021** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripotiti shuleni mara moja baada ya orodha ya waliochaguliwa kutolewa
2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**
 - a) **Sare ya shule**
 1. **WASICHANA**
 - (i) Sare ya shule hii ni sketi mbili, moja ya kijani iliyoiva (kitambaa kizito) na moja ya zambarau iliyoiva (kitambaa kizito). Sketi iwe ndefu inayofika chini na kugusa viatu. Mashati mawili meupe mikono mifupi
 - (ii) Tai moja ya kijani na moja ya zambarau iliyoiva
 - (iii) Rangi ya hijab(kijuba) iwe nyeupe tu
 - (iv) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suti rangi ya nyeusi na raba za michezo jozi moja
 - (v) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba na vyenye kisigino kifupi
 - (vi) Soksi jozi mbili nyeupe
 - (vii) Masweta mawili moja la zambarau iliyoiva na moja la kijani iliyoiva
 - (viii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni magauni mawili mshono wa solo (bajaji) blue draft na iwe ndefu mpaka chini
 - (ix) T-shirt inapatikana shule kwa gharama ya Tsh 10,000/=

2. WAVULANA

- (i) Sare ya shule hii ni suruali mbili, moja ya kijani iliyoiva (kitambaa kizito) na moja ya zambarau iliyoiva (kitambaa kizito). Suruali isiwe ya kubana (kushika mwili).
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
- (iii) Tai moja ya kijani na moja ya zambarau iliyoiva
- (iv) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suti rangi nyeusi na raba za michezo jozi moja
- (v) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba na vyenye kisigino kifupi
- (vi) Soksi jozi mbili nyeupe
- (vii) Masweta mawili moja la zambarau iliyoiva na moja la kijani iliyoiva
- (viii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali ya khaki na isiwe ya kubana (kushika mwili)
- (ix) T-shirt inapatikana shule kwa gharama ya Tsh 10,000/=

b) VIFAA VYA TAALUMA

Kila mwanafunzi wakati wa kuripoti afike na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya masomo

- (i) Madaftari makubwa **tisa** (Counter book quire 2)
- (ii) Bunda (ream paper) moja la karatasi
- (iii) Mkebe (mathematical set) mmoja
- (iv) Kalamu ya wino
- (v) Kalamu ya risasi
- (vi) Dawati na kiti cha chuma

c) HOSTELI

Shule inayohuduma ya hosteli kwa wavulana na wasichana. Hosteli hii inaendeshwa kwa michango ya wazazi/walezi wa wanafunzi wanaokaa hapa. Pamoja na mahitaji ya kibinadamu kila mwanafunzi anatakiwa kukamilisha michango ifuatayo:

- (i) Mahindi gunia moja kwa muhula mmoja
- (ii) Maharage debe moja na nusu kwa muhula mmoja
- (iii) Fedha taslimu Tsh 50,000/- kwa muhula
- (iv) Vifaa vya chakula na malazi
 - (a) Godoro futi mbili na nusu moja
 - (b) Shuka mbili rangi ya pink
 - (c) Sanduku la chuma (Tranka) moja
 - (d) Sahani moja, bakuli moja, kijiko kimoja

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani nje ya maelekezo hapo juu na siku ya kuripoti avae tracksuit nyeusi. sare za shule ataanza kuzivaa baada ya kukaguliwa na kupokea maelekezo

d) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

- (i) Ream ya karatasi moja (kwa mwaka)
- (ii) Kamusi (Dictionary) moja
- (iii) Godoro moja kwa mwanafunzi wa hostel
- (iv) Mashuka mawili rangi ya pink, blanketi moja, foronya na chandarua kimoja
- (v) Vyombo vya chakula (sahani moja, bakuli, kikombe cha nusu lita na kijiko)
- (vi) Ndoo mbili (kubwa moja na ndogo moja) zenye mifuniko kwa mwanafunzi wa hostel
- (vii) Vifaa vya usafi (jembe moja, kwanja moja na mifagio wa chelewa)

3. MAKOSA YATATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZA SHULE

- (i) Wizi
- (ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/utoro
- (iii) Kugoma au kusababisha mgomo
- (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
- (v) Kupigana (mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule)
- (vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanaakiwa kuwa nanywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
- (vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- (viii) Uvutaji wa sigara
- (ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuolewa
- (x) Kupata ujauzito au kutoa mimba
- (xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi
- (xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- (xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- (xiv) Kudharau bendera ya Taifa
- (xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
- (xvi) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi

4. Viambatanisho na fomu muhimu

- (a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination form)
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai
- (c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango iliyokubaliwa katika vikao rasmi na maelekezo yote yatakayotolewa na shule

5. Tafadhari soma kwa umakini maelezo/ maagizo haya na kuyatekelza kikamilifu

KARIBU SANA MPUI SEKONDARI

.....

**EDDAH MBUBA
MKUU WA SHULE**

OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA
SHULE YA SEKONDARI MPUI
MKATABA

Unatakiwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu.

SEHEMU A : MWANAFUNZI

Mimi.....nimesoma na kuelewa vizuri sheria, maagizo na kanuni zote za shule, nakubali/ sikubali nafasi hii na kuwa uwezo wangu wote kujiendeleza kitaaluma, nitatii sheria ,maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katiaka mgomo,fujona makosa ya jinai.

Saini.....

Tarehe.....

SEHEMU B: MZAZI /MLEZI

Mimi.....mzazi /mlezi wa.....nimepokea tgaarifa ya mwangu ya kujiunga na shule ya sekondari MPUI. Kwa kutambua umuhimu wa elimu na wajibu wangu, naahidi kuwa muda wote mwanangu atakapo kuwa shuleni nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea motto kwa k,ufuata sheria ,maagizona kanuni zoteza shulena kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya shule,nitatekeleza yote yatakayaotolewa na shule na nnitatoa ada na michango mingine yote ya shuleiliyopitishwa kwa wakati.

Saini.....

Tarehe.....

SUMBAWANGA DISTRICT COUNCIL

MPUI HIGH SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants

Student's full name.....

AgeYearsSex

Blood count (red and white)

Stool examination

Urine analysis, syphilis and other venereal diseases test

.....

T.B test

Eye test.....

Ears

Abdomen

Urine for plant test.....

Test for pregnancy

ADDITIONAL INFORMATION

Defects, impotents (e.g arms, legs etc) infections, chronic or family disease etc

.....
.....
.....
.....

I certify that the named above is fit to pursue further studies and domestic education

StationSignature

DateDesignation

SHULE YA SEKONDARI MPUI - SUMBAWANGA
FOMU YA KUANDIKISHA HABARI ZA MZAZI

Jina kamili.....

Tarehe ya kuzaliwa.....

Dini.....

Uraia.....

Anwani ya nyumbani.....

Simu ya baba.....

Simu ya mama.....

Simu ya mtendaji wa mtaa au kijij.....

Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwanafunzi

.....
.....
.....
.....
.....

Nathibitisha kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni kamili na kweli